*Nordic Journal of African Studies 9(2): 49-59 (2000)*

# Usimulizi wa Riwaya ya Nyongo Mkalia Ini

E. S. MOHOCHI
*University of Egerton, Kenya*

## UTANGULIZI

Tukichunguza hazina ya uhakiki uliofanywa katika taaluma ya fasihi ya Kiswahili na kuiweka katika mizani, upande mmoja ubebe tahakiki zilizozingatia maudhui na mwingine zile zilizoangaza fani, upande wa maudhui utalemewa na uzito na kuanguka. Ni kweli kuwa umuhimu wa fasihi katika jamii unatokana na jinsi ambavyo inaimulika jamii na kuichora kwa madhumuni ya kuihakiki na kuirekebisha kutokana na udhati na uzito wa mafunzo mwafaka inayoyabeba. Ni kweli vile vile kuwa fasihi ni sanaa kutokana na matumizi ya pekee ya lugha na vipengele vingine vya fani ambavyo kwa pamoja huipa sura maalum na kuyafanya maudhui yake yatufikie katika hali na umbo linalovutia. Hali hii ndiyo huiwezesha fasihi kutuingia, ikatuchoma na kutufikirisha zaidi. Ndio nguzo ya utamu wa fasihi.

Katika misingi hiyo, uendelezaji wa fasihi; hasa kwa upande wa uhakiki unapaswa kuzingatia pande zote mbili za sarafu; yaani maudhui na fani inayoyabeba maudhui hayo. Makala hii imelengwa kutoa mchango huo kwa kuupa uzito upande wa fani ya fasihi kwa kuzingatia kipengele cha usimulizi. Nao uteuzi wa usimulizi umechochewa na ukweli kuwa mbinu hii haijachunguzwa na wahakiki wengi katika fasihi ya Kiswahili. Awali ya kuchambua jinsi ambavyo mbinu hii ya usimulizi imejitokeza katika riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini*, dhana ya usimulizi itafafanuliwa na nafasi yake katika fasihi kuwekwa bayana.

## 1. DHANA YA USIMULIZI

Katika masimulizi ya ngano, msimulizi ama fanani alijidhihirisha wazi wazi mbele ya hadhira yake. Kwa hivyo, kulikuwa na uhusiano, pamoja na mawasiliano ya moja kwa moja kati ya msimulizi na hadhira yake. Fanani aliweza hata kuwashirikisha wasikilizaji wake kwa kuwauliza maswali au hata kuwaimbisha sehemu za nyimbo zilizotumika katika masimulizi ya ngano. Hadhira nayo ilishiriki kwa kuitikia, kushangaa, au kusinzia, yote ambayo yalitoa ishara maalum kwa msimulizi.

Baada ya uvumbuzi wa maandishi kazi nyingi za fasihi zinapatikana katika maandishi na hivyo usimulizi dhahiri haujitokezi katika kazi hizo. Tunayategemea maandishi kuupata ujumbe wa wasanii ambao wakati mwingi hatuwafahamu. Ni wazi kwamba sifa nyingi ambazo zilipatikana katika uhusiano wa mtambaji na

hadhira yake haziwezekani hivi sasa, lakini bado swala la usimulizi ni la kimsingi sana katika uwasilishaji wa kazi mbalimbali za fasihi, hasa za nathari. Hatukosi kuisikia sauti ya msimulizi angalau katika akili zetu iwapo si katika masikio yetu pale tunapoifuatilia hadithi kwa kuisoma.

Kulingana na Attenbernd na Lewis (1963), usimulizi ni ule mkabala ambao hutuwezesha kuyatizama yanayotendeka na kusikia yanayozungumzwa katika kazi ya fasihi. Mlacha (1991), anauona usimulizi kama uhusiano uliopo baina ya msimulizi na hadithi yenyewe. Namna ambavyo msimulizi anaingiliana na hadithi, na nafasi yake katika uwasilishaji wa hadithi ndiyo hutuelekeza kufahamu usimulizi wake. Njia nzuri ya kuelewa hali hii ni kutambua ni nani anayetuwezesha kuipokea hadithi yenyewe; yaani matukio mbalimbali yanawasilishwa kwetu kwa kupitia kwa macho ya nani? Kimsingi, kuna maswali kadhaa ambayo huiweka wazi zaidi mbinu iliyotumika katika usimulizi. Ni vizuri kuelewa ni nani anayeisimulia kazi hiyo na ana mtazamo gani? Ana uhusiano gani na matukio ya hadithi husika? Jambo la muhimu katika swali hili ni uelewaji wa uhusika wa msimulizi. Anashiriki katika hayo matukio au la? Ni muhimu vile vile kuchunguza kama mtazamo wake wa matukio hayo ni wa kuaminika. Hayo ni baadhi tu ya maswala muhimu ambayo humsaidia msomaji wa kazi hiyo kuelewa msimulizi wake pamoja na mchango wake katika kuikamilisha.

## 2. MBINU ZA USIMULIZI

Kuna mbinu nyingi za usimulizi ambazo mwandishi anaweza kuzitumia kuiwasilisha kazi yake katika maandishi. Aina hizo za usimulizi hutofautiana kwa jinsi ambavyo zinazua athari tofauti kwa wasomaji. Kuna baadhi ambazo hutuongoza kumulika hisia zetu kwa msimulizi ilhali zingine hutuashiria kuangaza nadhari yetu kwa kile kinachosimuliwa. Kwa hivyo, mwandishi hupaswa kufanya uteuzi wa mbinu mwafaka ya usimulizi atakayoitumia kwa kutegemea yale anayonuia kuyasisitiza katika kazi yake.

### 2.1 USIMULIZI MAIZI

Msimulizi maizi pia huitwa msimulizi mwakote. Hawthorn (1985) anasema kuwa huenda mbinu hii ilikuwa tokeo la mojawapo ya sifa za Mungu ya kujua kila kitu. Mbinu hii ya usimulizi ndiyo kongwe zaidi kuliko mbinu nyingine za usimulizi. Tukikumbuka kuwa katika masimulizi ya ngano msimulizi alielewa kila kitu na hasa tabia zote za wahusika; inakuwa rahisi kuelewa ni kwa nini mbinu hii ni kongwe zaidi. Katika mbinu hii mwandishi huieleza hadithi ambayo, mara nyingi, yeye haimhusu; yaani haishiriki lakini, akiwa muumbi wake, anaelewa kila kitu kinachotendeka hadithini.

Msimulizi anakuwa na uhuru mwingi sana. Anajua kila kitu na ana nafasi ya kuamua yale atakayotuambia na yale atakayoyaacha. Ana uwezo wa kutamba na kueleza maswala mbalimbali; na usimulizi unaweza kutumia mhusika mmoja, halafu mwandishi akabadilisha na kutumia mhusika mwingine. Katika usimulizi huu, mwandishi ana uhuru kiasi kwamba tunamtarajia kuelewa hata mawazo ya wahusika wake. Kwa hivyo, msimulizi huingia katika akili ya mhusika na akatufafanulia mawazo yake, akatueleza hata kile ambacho mhusika anakikumbuka, na pia msimamo wake kuhusu maswala mbalimbali.

Kuna baadhi ya waandishi ambao wanaitumia mbinu hii kwa namna tofauti kidogo, na badala ya kutueleza tu mambo kuhusu hadithi , wanadokeza pia msimamo wao. Katika hali hii, mwandishi anaeleza mawazo au msimamo wa mhusika, anachanganua matendo yake na hata kufafanua wazi wazi kinachoyazua matendo hayo. Zaidi ya hayo, anaweza hata kutoa tathmini ya wahusika wake kwa kufafanua hulka zao (Attenbernd na Lewis 1963; Carpenter na Neumeyer 1974).

Kutokana na uhuru wake, mwandishi anaweza kutoa maelezo yote na kuingiza mambo mapya bila lazima ya kueleza jinsi alivyoyapata. Uelewaji wa kazi hiyo kwa upande wa wasomaji huwa umerahisishwa kwani msimulizi atatamba kote kule hadithi inatukia na kuyaweka wazi matukio yote. Mwandishi anapotumia mfumo tulioutaja wa kutoa msimamo wake mara kwa mara anakumbusha wasomaji kuwa ndiye ameibuni na wala wayasomayo si matukio ya kikweli; hasa iwapo wanamfahamu mwandishi mwenyewe. Kwa upande mwingine, matukio yanaposimuliwa bila kutolewa maelezo na mwandishi, kuna uwezekano mkubwa sana wa wasomaji kutekwa na matukio hayo yanayojipambanua yenyewe bila kumkumbuka mwandishi. Mbinu ya msimulizi kutoa msimamo wake kuwahusu wahusika au matendo yao ("editorial omniscience") inamfanya aingilie kati badala ya kuwaachia wasomaji nafasi ya kutafakari na kujiamulia wenyewe.

## 2.2 Usimulizi wa Nafsi ya Tatu

Katika usimulizi huu mwandishi anasimulia akitumia nafsi ya tatu lakini anajikita zaidi katika mhusika mmoja tu. Anajibana na kujipunguzia anayoyafahamu kwa kudhihirisha ufahamu wa mhusika mmoja peke yake. Yote anayoyajua ni kumhusu huyo mhusika na haonyeshi kuwafahamu wahusika wake wengine. Kwa hivyo, mawazo, mwelekeo na msimamo wa mhusika huyo mmoja ndio mwandishi anaoutambua kwa undani. Hapa mwandishi huwa amejipunguzia uhuru wake wa kuyaeleza yote anayoyajua kuihusu hadithi yake. Mhusika anayepewa nafasi hiyo aweza kuwa mhusika mkuu au mhusika mwingine yeyote hadithini.

Kulingana na S. A. Mohamed (1995) usimulizi wa nafsi ya tatu ni ule unaompatia mhusika mmoja nafasi ya kusimulia hadithi badala ya msimulizi mwakote kuisimulia yote. Ametoa mfano wa bwana Msa wa Mohamed S. Abdalla (1976) ambaye hupewa wakati kuendeleza masimulizi ya hadithi na kusimamia mawazo ya mwandishi. Jambo muhimu linaloibuka kutokana na mawazo ya

Mohamed ni kuwa mbinu za masimulizi zaweza kuchanganywa katika kazi moja ya fasihi.

## 2.3 Usimulizi wa Nafsi ya Kwanza

Katika mbinu hii ya usimulizi mwandishi hupotelea ndani ya mmoja wa wahusika wake ambaye husimulia hadithi yote. Mohamed (1995) anasema kuwa mbinu hii si rahisi kama inavyoonekana kwani mwandishi anapaswa kuwa makini asitumie ‘ni’ na ‘mimi’ kwa wingi hadi akawachosha wasomaji wake. Japo mbinu hii haijatumika sana katika fasihi ya Kiswahili, kuna mifano ya hapa na pale.

Msokile (1981) ana hadithi ya “Roho Nyeusi” inayoanza hivi:

> Nayainua macho yangu kwa mara nyingine na kumwangalia Beata kwa hasira huku kimoyo chake kitete kikidunda taratibu kifuani pake¼(uk. 49)

Aidha, Ruhumbika, katika hadithi ya “Wali wa Ndevu”, *Parapanda,* anatumia mbinu hii:

> ¼Si nia yangu kusimulia tena maajabu tuliyoyaona visiwani, majumba malidadi ajabu ya kukaa , bure, wananchi, mabarabara safi ya kisasa¼.(uk. 63)

Mifano hiyo miwili inadhihirisha kuwa masimulizi katika hadithi hizo yanafanywa katika nafsi ya kwanza. Mbinu hii inawasilisha hadithi kama ambayo imesimuliwa na mmoja wa wahusika wake. Kunakuwa na matumizi ya ‘ni’; kiwakilishi nafsi ya kwanza. Mhusika anaweza kuwa nguli (“Roho Nyeusi”) ambaye anasimulia hadithi yake mwenyewe, ama akawa mhusika mdogo tu akieleza yaliyomkumba nguli. Kwa mfano, katika “Wali wa Ndevu” msimulizi wake ni mhusika mdogo tu.

Usimulizi huu humbana sana mwandishi kwani kuna mambo mengi sana ambayo hawezi akayaeleza bayana. Kwa mfano, mawazo ya wahusika wake wengine hayatatufikia vilivyo. Itaonekana kuwa katika hali hii tunalazimika kutizama mambo kupitia kwa mtu mmoja, tunayemtegemea kutueleza mambo ambayo hatuyashuhudii wenyewe. Mwandishi anaweza kuamua kutumia mazungumzo baina ya wahusika, barua au mbinu nyingine ili kutupanulia mtazamo wa kazi yake.

Carpenter na Neumeyer (1974: 184) wanatoa mawazo yafuatayo kuihusu mbinu hii:

> Wasomaji wanagenzi huweza wakachukulia kuwa msimulizi wa nafsi ya kwanza ana mawazo sawa na ya mwandishi. Si lazima iwe hivyo na wakati mwingine mawazo yake ni kinyume kabisa na yale ya mwandishi mwenyewe.

Kwa hivyo ni makosa kuyaoanisha mawazo ya msimulizi wa nafsi ya kwanza na yale ya mwandishi kwani msimulizi kama huyo ni mhusika kama wale wengine hadithini na wala si lazima awe msemaji wa mwandishi. Hata hivyo, mbinu hii ina faida zake. Wakati mwingine mwandishi hutaka tuutizame ulimwengu wake kupitia

kwa mhusika maalum, kama vile kijana mdogo, mama mzee, na kadhalika. Tuyaelewe maisha kupitia kwa mtazamo wa aina fulani ya wahusika. Kwa baadhi, hadithi inayotumia usimulizi wa nafsi ya kwanza huwa hai zaidi kwani huifanya hadithi ifanane na maisha ya kila siku.

Vile vile katika usimulizi huu mwandishi huficha mambo ambayo msimulizi wake hayatambui mpaka pale ambapo yatahitajika katika maendeleo ya ploti, hasa katika hadithi za upelelezi.

## 3. USIMULIZI WA NYONGO MKALIA INI

Kila hadithi ina mwandishi. Aidha, ina msimulizi ambaye yuaweza kuwa mwandishi ama mtu mwingine ambaye mwandishi anamwelewa vilivyo (Mlacha 1991). Sehemu hii itatalii namna ambavyo mwandishi Rocha Chimerah (1995) amesimulia hadithi yake. Rocha si mgeni katika uandishi wa Kiswahili. Kando na riwaya hii, mwandishi huyu amechapisha vitabu kadhaa, vikiwemo; *Kiswahili Past, Present and Future Horizons, na Mnara Wawaka Moto*. Ameshirikiana na waandishi wengine kuandika vitabu mbalimbali. Aidha, Chimerah amechapisha makala kadhaa kuhusu lugha na fasihi ya Kiswahili.

Akiwanukuu Leech na Short (Mlacha 1991) anasisitiza swala la umuhimu wa kujenga uhusiano baina ya mwandishi na hadhira yake ili anayoyaeleza yapambanuliwe na kueleweka vyema. Ni sharti mtunzi katika kuumba na kuwasilisha kazi yake, awafikirie wasomaji wake pamoja na kuzingatia njia bora ya kuwawezesha kuipokea hadithi yake. Hili huathiri uteuzi wake wa njia ya usimulizi.

Hadithi hii ya *Nyongo Mkalia Ini* imesimuliwa zaidi kwa kuelemea katika mbinu ya nafsi ya kwanza. Hii hapa mifano ya kudhihirisha hali hiyo.

> Nilinyanyua uso wangu nikariaria huku na huku. Ndio mwanzo niwatambue haswa wenzangu tuliomo sote humu chumbani... (uk. 1)
>
> ...ikiwa bado una shaka, maelezo yangu ya mwisho ni kwamba hoteli hii i katikati ya Baraste ya Makadara. (uk. 8)
>
> Nikisema nilipata usingizi wa haja, nadanganya. (uk. 95)

Matumizi haya ya viwakilishi mbalimbali vya nafsi ya kwanza ni dhihirisho kuwa riwaya hii inasimuliwa na mmoja wa wahusika wake katika nafsi ya kwanza. Anavyoonya Mohamed (1995), mwandishi anapoteua kutumia mbinu hii anapaswa kuwa makini sana ili asitumie hizo "ni" na "mimi" kiholela na kwa wingi kiasi cha kuwachosha wasomaji wake. Kwa hivyo mbinu hii, kinyume na imani ya watu, si rahisi kuitumia pasipo kukinai wasomaji.

Mbinu hii hupelekea waandishi kujaribu kutuelekeza kuona kuwa anayesimulia hadithi ni mtu mwingine kabisa na wala siye. Hili wanalitekeleza kwa kujaribu

kujitenga na wasimulizi kwa kuwataja wahusika wasimulizi kwa majina. Hivyo, msomaji anabaki kudhania tu kuwa mwandishi ndiye huyo mhusika. Katika hali hii, mwandishi anatoa rai na maoni yake kama mmoja wa wahusika wa hadithi. Licha ya hali hiyo ya waandishi kutaka kujitenga na msimulizi wa hadithi zao, ukweli ni kuwa kutokana na hali kwamba hadithi yenyewe ni utunzi wa waandishi, tunapozifuatilia hadithi nzima yale matumizi ya nafsi ya kwanza, kinyume na kututenganishia mwandishi na msimulizi, kama anavyodai Mlacha (1991: 60), yanatuongoza zaidi kutizama hadithi hiyo kama inayosimuliwa na mwandishi mwenyewe. Swala la mhusika msimulizi kupewa jina tofauti na la mwandishi halitufungi macho kwa sababu tunaelewa kuwa mwandishi ana uhuru wa kutumia majina ya kubuni huku akirejelea mambo mahsusi. Vivyo hivyo, yuaweza kujibandika jina la kisanaa.

Kutona na utata huo, mawazo ya Carpenter na Neumeyer (1974: 184) kuhusu mbinu hii ni mwafaka sana. Wanaonya kuwa ni sharti wasomaji tutahadhari tusije tukayachukulia mawazo ya msimulizi kuwa sawa na ya mwandishi kwani wakati mwingine huwa ni kinyume kabisa.

Tuendelee kuchunguza jinsi Rocha Chimerah alivyoitumia mbinu hii. Katika riwaya hii, Rocha ameamua kumtumia mhusika Juma Momanyi kama kinara anayetuongoza kufuata hadithi yake. Kwa hivyo, wasomaji twapaswa kuwa waangalifu tusije tukayachukua maoni, msimamo na imani zote za Juma kuwa kiwakilishi cha maoni, msimamo na imani za Rocha.

Mbinu hii inapotumika, tunalazimika kufuatilia matukio, kuwafahamu wahusika wengine na kuielewa hadithi kwa jumla kupitia kwa jicho la huyo mhusika msimulizi. Msimulizi ndiye anatembea kote na kutufunulia mengi kuhusu mandhari, wahusika n.k. Kwa mfano, anatufahamisha barabara ilivyo nyumba ya Omari;

> Chumba cha kwanza mkono wa kulia uingiapo ni msala, cha pili ni jiko. Cha tatu ndicho chumba cha Omari... (uk. 48)

Aidha, ndiye anayetuingiza katika ofisi ya bwana Khalifa na kutufahamisha ilivyo - mapambo yake na vyote vilivyomo.

Katika uk.1, Juma anatueleza hali ya Omari aliyelala kitandani mgonjwa aso hali kisha anageukia wengine waliomo mle chumbani. Katika mbinu hii msimulizi anafanya jambo moja kwa wakati maalum, kisha akageukia jingine. Tunamtegemea yeye kuelewa mengi kuihusu hadithi nzima.

Mbinu hii ya usimulizi humbana sana mwandishi. Msimulizi anatueleza na kutufahamisha yale anayoyashiriki tu (ama kwa kuambiwa, kusikia au kuona). Ni lazima msimulizi awepo, atueleze. Vinginevyo hatuna namna ya kujua kinachoendelea pale ambapo msimulizi wetu hajafika. Kwa mfano, kwa vile hayuko chuoni Gachuka hawezi kutufahamisha yanayoendelea huko. Ndiposa mwandishi alipohitaji kutufahamisha yanayoendelea huko akalazimika kutumia barua ya Munga kutujulisha hayo. Pamoja na hayo bado tunamtegemea Juma kwani hata barua hiyo aliyeandikiwa ni yeye.

Mwandishi anapoeleza jambo fulani mahali maalum, hawezi akaeleza linaloendelea kwingineko, tofauti na mwakote anayeona na kusikia, pamoja na kuingia kila mahali. Iwapo mbinu tofauti ingetumika katika riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini,* mwandishi angeweza kutuhamisha kutoka Uziwani hadi Gachuka, akawaacha wa Uziwani kiporo na kutudhihirishia mapambano ya wanafunzi wa zutafundaki na askari polisi, kisha akaturegesha Uziwani. Angekuwa msimulizi maizi, yatendekayo sehemu mbalimbali hutufikia kwani msimulizi huyo yu pote wakati wote.

Matokeo ya matumizi ya usimulizi wa nafsi ya kwanza ni kwamba riwaya hii imejaa maelezo marefu marefu kuhusu mambo mbalimbali. Yapo maelezo kuwahusu wahusika kama mama Mumbe, Warega, maumbile yao, sifa, pamoja na tabia zao mbalimbali. Maelezo kuhusu mandhari ambamo matukio ya hadithi hii yanatukia, ndoto ndefu ndefu za Juma Momanyi, maelezo kuhusu matukio mbalimbali ya kihistoria n.k. Tatizo kuu la matumizi ya maelezo marefu sana ni hatari ya kuwachosha wasomaji wa kazi maalum.

Hata hivyo, mwandishi ameitumia vyema mbinu hii kwa sababu ameichanganya na ubunifu wake mwenyewe ambao unaipa ubora wa namna yake. Kwanza kabisa, si Mumanyi tu anayepewa jukumu la kusimulia mambo yote. Kama kawaida ya kazi mbalimbali za fasihi, kuna mahali kwingi mno ambapo wahusika zaidi ya wawili wanazungumza kwa kujibizana na hilo si kwa kuendeleza ploti ya riwaya hii tu bali pia kuwafafanua wahusika wenzao na kadhalika. Pili, pale ambapo panahitajika maelezo marefu ya kisimulizi, wapo wahusika wengine ambao pia wameshirikishwa. Wapo Warega, mama Mumbe, pamoja na Amu Zaid, japo masimulizi yao ni mafupi kidogo yanapolinganishwa na yale yanayofanywa na Mumanyi. Kwa mfano maelezo yatolewayo na mama Mumbe na hatimaye mwanae Warega kuhusu vita vya uhuru na mateso mengi waliyopatishwa wazalendo yametolewa kwa namna nzuri sana. Maelezo haya yanamteka msomaji na kumfanya ahisi mpwitompwito mwilini kwa kuwahurumia wale waliojitoa mhanga kwa ajili ya nchi yao.

Mara kwa mara, katika usimulizi huu wa nafsi ya kwanza, mwandishi ametumia mbinu ya kuuliza swali au kuulizwa swali; hali nzuri ambayo inatoa fursa kwa wale wahusika wengine kushiriki kikamilifu hadithini na kukata maelezo ya mfululizo wa moja kwa moja. Kwa mfano;

> Sijaacha kukuuliza. Umesema penye sultani ama mfalme hapana kura...Mbona huko Ingereza serikali ina vyama viwili vinavyokinzana kila muhula ilhali twajua Ingereza yatawaliwa na malkia? (uk. 75)

Aidha, matumizi ya barua ya Munga pamoja na ile ya D. Chipuli Dzuya katika gazeti la *'Baraza'* ni namna nzuri sana ya kuchanganya na masimulizi ya moja kwa moja ili kuendeleza ploti bila kuwakinai wasomaji. Barua hizi vile vile zinatekeleza jukumu muhimu la kuwaingiza wahusika walio mbali katika hadithi hii.

Swala jingine muhimu linaloibuka katika usimulizi wa *Nyongo Mkalia Ini,* ni ile hali ya usimulizi wa kingano ambapo msimulizi ama mtambaji aliwasiliana moja

kwa moja na hadhira yake. Katika riwaya hii msimulizi naye, mara kwa mara, anawasiliana na hadhira yake ya ama wahusika wengine hadithini au wasomaji wake. Katika uk.16 anawasiliana na wahusika wenzake kwa kusema yafuatayo;

> Nyote mwakumbuka vyema siku za mwanzo mama Mumbe alipoingia mjini na bintiye Warega...

Hili linatukumbusha ule mtindo wa usimulizi wa ngano ambapo msimulizi alidhihirika wazi wazi mbele ya wasikilizaji wake, akawasiliana nao moja kwa moja na hata kuwashirikisha katika masimulizi yake ya hadithi. Huu ndio mtindo ambao wametumia Ama A. Aidoo katika hadithi ya *"In the cutting of a Drink"* (1985) pamoja na Ngugi wa Thiong'o katika *"A Mercedes Funeral"*.

Kwingineko riwayani (uk. 47), baada ya kuwasimulia kisa fulani, Mumanyi anawauliza wahusika wengine waliokuwepo hivi;

> Ni nani aliye tayari kukitegua kitendawili hicho?....

Aidha, upo wakati hadithini ambapo mwandishi kupitia kwa msimulizi wake anajaribu kuwasiliana moja kwa moja na wasomaji wake. Huu hapa mfano wa hali hiyo;

> Tulirudishwa kichekoni. Tulipopoa Warega akachukua uwanja... (uk. 82)

Hapo ni bayana kwamba msimulizi amejiunga na wahusika wenzake na kutufahamisha walichokuwa wakikitenda wao kwa pamoja.

Foster (Mlacha 1991) anasema kuwa mwandishi ana uwezo wa kuzungumza kuhusu wahusika wake au kuzungumza kupitia kwa wahusika wake. Yapo mawazo mazito, na ya kikauli yanayotolewa na Rocha kupitia kwa wahusika wake mbalimbali. Kwa mfano, amemtumia mhusika Munga pamoja na Juma kutoa kauli madhubuti na za kimsingi sana kuhusiana na imani ya muda mrefu kuhusu watu wa pwani, ambao yasemekana, ni wavivu. Ukizipitia kauli hizi na zingine kwa makini hutakosa kung'amua kuwa haya ni mawazo au maoni ya Rocha Chimerah kuhusu maswala mbalimbali yaihusuyo jamii anayoyamulika katika riwaya yake.

Dosari moja kuu ninayoiona kuhusiana na usimulizi wa nafsi ya kwanza ni kwamba mbinu hii yaweza kukinai na kuchosha, tofauti na nyingine ambazo zinatoa nafasi kubwa kwa watu wengi kushiriki kuiendeleza hadithi. Hili linajitokeza katika *Nyongo Mkalia Ini*, hasa pale ambapo mwandishi anatumia msimulizi wake kutuelekeza kutizama mambo anavyotaka yeye. Kwa mfano;

> Sasa hebu niifungue nione ananieleza kisa gani... (uk. 15)

Hapa, msimulizi anatuelekeza na kutuongoza, hali ambayo inaikatisha furaha yetu kama wasomaji ambayo tungeipata iwapo angeendelea na masimulizi kisha sisi wenyewe tuunge vijisehemu vijitokezavyo na hivyo kujigundulia mshikamano wa kadhia yake.

Katika uk. 45, msimulizi wa *Nyongo Mkali Ini* anatoa maelezo kuhusu swala la nyuki walao asali, pamoja na ile ndoto yake. Juma anayahitimisha maelezo hayo hivi:

> Mja...nyuki...Samahani ndugu; huo ndio utakao kuwa mwisho wa maelezo yangu juu ya nyuki...

Ufafanuzi huo haukuwakolea wasikilizaji wake; nao wakataka maelezo zaidi. Bila kusita akajibu;

> Haya basi nitajaribu kufafanua zaidi...Sisi sote ni nyuki. Kama nyuki tumegawanyika matabaka matabaka. Kama nyuki, wapo wanaochuma asali na wanaokula asali. Ni wajibu wa kila... afadhali tutie kikomo hapo. (uk. 46)

Ukweli ni kwamba hii kauli yake inadhihirisha vizuri sana namna ambavyo jamii yetu imegawanywa katika matabaka huku wachache wanafurahia jasho la wengi. Kwa hilo, sawa kabisa, lakini ingekuwa bora kama angetufumbia na kutuacha wenyewe kujijazia. Unapofumba na kisha ukataka kutanzua au kulifumbua fumbo, ile raha ya fasihi inakuwa haipo tena. Ingawa anaghairi kuendelea kulifafanua fumbo lake; hivyo kutuachia jukumu letu kama wasomaji, hafanyi hivyo kwa sababu anaamini si vizuri, bali kwa sababu, kama asemavyo mwenyewe; "hata nyasi zina masikio". Ni maswala nyeti ambayo hayapaswi kuelezwa wazi wazi.

Tatizo jingine ni lile la msimulizi kutoa maelezo mengi kujihusu. Katika kuwafafanua wahusika, mbinu ya mhusika kujieleza mwenyewe si nzuri sana kwa sababu huenda akatuficha mengi ambayo hataki tuyajue kama ilivyo kawaida ya mwanadamu. Hii hapa mifano miwili ya jinsi msimulizi anavyojitathmini:

> Kwa kawaida huwa sipendi kuingiaingia mabaani...na mimi sipendezwi na baa yoyote hata kama ina sifa za uzuri wa peponi. (uk. 8)
>
> ... sijisifu, lakini kwa kuwa ni mwenye kupenda ukweli, nasema kweli... (uk. 1)

Utaona kuwa msimulizi anatueleza yale atakayo yeye, sisi tuyajue na kuacha asiyoyataka. Kwa kufanya hivyo, anatuelekeza katika mkondo maalum wa mawazo anaoupendelea yeye. Japo anaonya kwamba hajisifu; ukweli ni kwamba ndivyo anavyofanya. Ingekuwa bora kama tungepata kukaulisha kuhusu hulka yake na sifa zake mbalimbali kutokana na maingiliano yake na wahusika wengine hadithini, matendo yake, pamoja na wanayoyasema wahusika wengine badala ya kuambiwa naye.

## 4. HITIMISHO

Kwa jumla, pamoja na matatizo mbalimbali yanayoambatanishwa na mbinu hii ya usimulizi, mwandishi wa riwaya hii ameitumia vizuri. Ameweza kutumia ubunilizi wake mwenyewe kuepuka ukinai wa usimulizi wa nafsi ya kwanza. Amefanya la busara pia kuwapa wahusika wengine kando na Juma (msimulizi mkuu), nafasi ya kusukuma mbele hadithi yake. Hali hii tunaishuhudia zaidi wakati wa majadiliano marefu yanayowakutanisha Munga, Obote, Omari, Warega, pamoja na Mumanyi mwenyewe.

Hilo pamoja na matumizi mazuri ya hadithi za mama Mumbe, maelezo ya Warega pamwe na zile barua zipatikanazo katika riwaya hii linaipa kazi hii upekee katika matumizi ya usimulizi wa nafsi ya kwanza. Aidha, hayo yamemsaidia mwandishi kuepuka tata mbalimbali na ukinai wa usimulizi wa nafsi ya kwanza, hasa itokeapo kwamba usimulizi huo haujachanganywa na mbinu nyingine zozote wala kuambatanishwa na ubunifu wa mwandishi husika.

## MAREJELEO


Abdalla, M. S. 1976.
Kuandika Hadithi za Kubuni. Katika *Uandishi wa Tanzania: Insha,* East African Literature Bureau, Nairobi.

Aidoo A. A. 1985.
In the Cutting of a Drink. Katika *African Short Stories: An Anthology.* Mcmillan Kenya, Nairobi.

Attenbernd, L. & Lewis, L. L.(wh.) 1963.
*Introduction to Literature: Stories*, Macmillan Company, New York.

Carpenter, J. na Neumeyer, P. 1974.
*Elements of Fiction: Introduction to the Short Story.* W.M.C. Brown Company Publishers, Dubuque, Iowa.

Chimerah, R. M. 1995.
*Nyongo Mkalia Ini.* Nairobi University Press, Nairobi.

Hawthorn, J. 1985.
*Studying the Novel: An Introduction*, Universal Book Stall, New Delhi.

Mlacha, S. A. K. 1991.
Point of view as Stylistic Device in Kiswahili Novels. **Kiswahili** Vol. 58. TUKI, Dar es Salaam.

Mohamed, S .A. 1995.
*Kunga za Nathari ya Kiswahili*, East African Educational Publishers, Nairobi.

Msokile, M. 1981.
*Nitakuja kwa Siri*. Dar es Salaam University Press, Dar es Salaam.
Ruhumbika, G. (mh.) 1982.
*Parapanda*. East African Publications Limited, Arusha.